Kongamano la Kiswahili Bayreuth

UNIVERSITÄT BAYREUTH

Mwaliko wa

# KONGAMANO LA KUADHIMISHA MIAKA THELATHINI

Bayreuth Tarehe 26 hadi 28 Mei 2017

Wenzetu wapendwa, wapendwa washiriki, ndugu na marafiki,

Tuna furaha kubwa kuwakaribisheni kusherekea miaka thelathini ya Kongamano la Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Bayreuth! Kwa furaha tunatayarisha kongamano la 2017 litakaloadhimisha miaka thelathini tangu kuanzishwa! Tangu hapo mwaka wa 1987, ambapo kongamano la kwanza lilifanyika ili kusherehekea miaka 100 ya ufundishaji wa Kiswahili vyuoni hapa nchini Ujerumani, Kongamano la Kiswahili limepiga hatua nyingi.

Leo hii, kongamano hili ni mkutano wa kipekee wa kila mwaka, utoao fursa kwa yeyote yule aliye mtaalamu wa masomo mbalimbali yanayohusu utafiti na uchunguzi wa vipengele kadha wa kadha vya lugha, fasihi na tamaduni za Afrika Mashariki. Msingi huu wa kongamano letu mjini Bayreuth, unaojikita katika nyanja na mada maridhawa, huwa ni fursa kwa wengi kujuzana kuhusu tafiti zinazoendelea. Hivyo basi, tunawakaribisheni tena wote ambao huja hapa Bayreuth katika miaka iliyopita na pia tutafurahi sana kuwapokea na kuwakaribisha wataalamu, wanafunzi na mashabiki wapya katika kongamano lijalo.

## Mada kuu ya kongamano la 2017

Kongamano la Kiswahili la 2017, lililo la kuadhimisha miaka thelathini, litawarejelea wataalamu na wasomi walioliwezesha kufanikiwa na kuota mizizi. Tutafurahi pia, kujumuika na *wanakizazi kipya*, ili pamoja tumulike taaluma za Kiswahili kiundani, tutathmini hali ilivyo, tujadili nafasi na changamoto zake na kutabiri yajayo.

Tungependa kupata makala yanayohusu mitazamo ya kihistoria na mitazamo iangaliayo siku zijazo katika mustakabali wa taaluma za Kiswahili. Katika mada hii, kichwa cha wito wa kongamano la 2017 ni: **“Mahusiano! Lugha na fasihi katika maingiliano”**.

Katika uhalisi wa Afrika Mashariki, kuna miseto ya lugha na tamaduni. Uhalisi huu pia una mikondo ya uhamaji na athari za utandawazi. Katika hali hii, lugha na fasihi haziwi bila ya kuathiriwa na miseto hiyo. Nyanja mbali mbali za hali halisi na miseto hiyo huathiriana na kuathiri lugha na fasihi. Hatima ya hali hii ni kwamba, sarufi na fasihi mbadala, ambazo ni matokeo ya athari za lugha jirani, huzuka na kuzidi kuongezeka. Kwa mfano, bahari tofauti za fasihi huzuka na kukubalika hususan kwa mujibu wa uhusiano au upinzani ulioko baina yao (mfano wa riwaya na ngano); lugha fulani kupendelewa badala ya nyingine katika muktadha fulani; na vile vile, kuzuka kwa semi au matini zaidi ya moja na kutumika katika hali sambamba huku zikiigana na kukinzana. Tukizingatia wingi wa mafungamano, ulinganifu, uwiano, ubadilishanaji na ubunifu; ulio kigezo msingi katika utoaji/utunzi wa fani mbalimbali za kitamaduni, kuwa ndio mwanzo wa majadiliano yetu, tunawakaribisha kuchangia katika nyanja tofauti za taaluma zinazochunguza jinsi ya kusambaa, kupokea, kumiliki na kusambaza upya ujuzi katika mazingira ya Kiswahili.

Tunapendekeza mtazamo ambao hauchukulii lugha na fasihi kama mfumo huru unaojisimamia, ila mtazamo unaouzingatia muktadha wa kuwepo kwa lugha mbalimbali na uwezekano kwa wazungumzaji, wasanii na waandishi kuchagua: Wazungumzaji huchaguaje rejista na lahaja fulani katika muktadha mahsusi? Mawasiliano ya kitamaduni huwezeshwa vipi wakati wa na katika hali ya maingiliano? Uhawilishaji kwa tafsiri, tafsiri huru na fasiri au matumizi ya *hypertext* yanawezeshaje fani za lugha na fasihi kusafiri ndani ya kundi moja au kutoka kundi moja hadi lingine na hivyo kuwezesha na hata kuanzisha uhusiano mpya? Maingiliano ya kitamaduni huchukua umbo, maana na kazi gani katika upokeaji, utoaji, uainishaji na utekelezaji wa ujuzi? Waandishi, waigizaji, wasanii na hadhira huafikianaje penye lugha na fani tofauti tofauti? Sera za uchapishaji zinamudu vipi, ongezeko la kila kuchapo, la njia za kusambazia fasihi pamoja na aina za hadhira?

Mtazamo katika mada kuu ya kongamano la 2017 unalenga kufanya uchunguzi unaotilia maanani dhana ya kuwepo kwa lugha na fasihi anuwai na hivyo kufanya utafiti wa uhusiano wa nyanja za lugha na fasihi ulioko kati ya Kiswahili na lugha zisizo Kiswahili. Tunataraji kuwa mitazamo mipya itazinduka kuhusu uchunguzi wa ushirikiano baina ya matumizi tofauti ya lugha, hazina za kifasihi, fani za vyombo vya habari, mifumo ya ishara na mifumo ya kufahamia au kung’amulia mambo ambayo huonesha taratibu ya njia zilizofuatwa katika uzukaji wa tamaduni fuatilizi. Itakuwa vizuri kama, tutapata mapendekezo ya paneli za wawasilishaji 2-4, makala ya mwasilishaji mmoja au njia yoyote ile angavu ya kuchangia katika mada hii.

Tumeshapokea pendekezo la paneli iitwayo “*Usimulizi na Uandishi kati ya mashairi ya mapokeo na mtiririko*”. Baada ya miaka arobaini ya mgogoro juu ya ushairi wa Kiswahili kati ya wanamapokeo na wanamageuzi, suala hili bado linawaka. Paneli hii inakaribisha mijadala kuhusu mahusiano kati ya mashairi (yote: simulizi na andishi) ya mapokeo na ya mtiririko. Paneli hiyo ingependa kutafakari aina ya misingi ya uandishi, upokeaji wa maandishi, ujumi wa matini, utafiti wa isimu ya matini, ufasaha wa mwandishi n.k.

Tumependekeza mada zilizo hapa juu ziwe ndizo mada kuu za kujengea mijadala yetu kwenye kongamano la 2017, lakini kama mjuavyo, Kongamano la Kiswahili Bayreuth halitaki kubana washiriki katika sehemu zilizotajwa tu. Kwa hiyo, pia tunawaulizeni msisite kupendekeza michango mingine ya vipengee vinavyorejelea lugha, fasihi au tamaduni za maeneo ya Kiswahili; kwani Kongamano la Bayreuth linalenga nyanja tofauti tofauti na vile vile ni fursa iliyo wazi kwa michango yoyote ile inayohusu Kiswahili, Uswahili na Waswahili kwa jumla.

**Usajili**

Tafadhali tumeni makala katika lugha ya Kiswahili au Kiingereza. Kila wasilisho litapewa muda wa dakika thelathini tu; ambamo dakika ishirini ni za kuwasilisha na dakika kumi ni za majadiliano na hadhira. Tafadhali jiandikishe kwa baruapepe kupitia *swahili@uni-bayreuth.de* na ututumie kichwa (angaa cha awali) cha makala au mapendekezo ya paneli mpaka **tarehe 30 mwezi wa Oktoba mwaka wa 2016**. Iwapo utawasilisha kwa Kiswahili, tutumie pia muhtasari wa makala kwa Kiingereza. Tunawaomba wote kujiandikisha hata ikiwa mtashiriki bila ya kuwasilisha makala.

**Pahala na Wakati**

Pahala pa Kongamano hili ni Iwalewahaus, kituo cha masomo ya Kiafrika ya Chuo Kikuu cha Bayreuth, iliyoko kwenye Wölfelstraße 2, kuanzia tarehe 26 Mai hadi 28 Mai 2017.

Wasilianeni nasi bila kusita iwapo mna maswali yoyote. Kwa mambo yote yanayohusu kongamano tafadhali tumieni anwani yake ya barua pepe; yaani *swahili@uni-bayreuth.de*

Karibuni nyote!
Salamu nyingi,
Ni watayarishi wenu
Serena Talento, Nikitta Adjirakor, Fred Bosire, Roberto Gaudioso, Annachiara Raia, Serena Talento, Rosanna Tramutoli na Clarissa Vierke

Swahili Colloquium
Prof. Dr. Clarissa Vierke
Literaturen in afrikanischen Sprachen
Universität Bayreuth
95440 Bayreuth
Telefon: + 49 921 55-3550
Fax: + 49 921 55-3641
Email: swahili@uni-bayreuth.de
http://www.afrikanistik.uni-bayreuth.de/de/colloq/swahili_colloq/